## FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL1

## KISWAHILI PAPER 3 QUESTIONS

# SEHEMU YA A (Alama 20 )

### KIDAGAA KIMEMWOZEA - Ken Walibora

1. **SWALI LA LAZIMA**

"Dunia imepasuka ufa mkubwa usiozibika alaa kulihali…"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Fafanua mbinu mbili za lugha zilizotumika katika dondoo hili (alama 4)

c) Thibitisha ukweli kuwa 'dunia imepasuka ufa mkubwa' kwa kumulika matukio sita riwayani. (alama 12)

# SEHEMU YA B (Alama 20 )

### TAMTHILIA MSTAHIKI MEYA -Timothy M. Arege

2. **Jibu swali la pili au la tatu.**

2. Mhusika mstahiki Meya na daktari Siki ni ndugu lakini tofauti zao ni kama ardhi na mbingu. Thibitisha kwa kutoa mifano kutoka kwa tamthilia.

(alama 20)

**au**

3. "Yaliyotuleta hapa kwa sasa umeyasikia"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama4)

4) b) Kwa kutoa mifano minne mwafaka fafanua mambo ambayo msemewa alikuwa ameyasikia. (alama 8)

c) Jadili madhara yaliyotokana na msemewa kuyapuuza malalamishi ya msemaji. (alama 8)

# SEHEMU YA C (Alama 20 )

### USHAIRI

3. **Jibu swali la 4 au la 5 4.**

**4. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

EL-NINO
El-nino, harufuyo yatughasi, tangazo lako, ni vilio huvileta.

El-nino, hushtushwa na unyasi, ambaye nyoka, awali alining'ata

El-nino, vua tesi la nafusi, maafa yako, hayatupaki mafuta.

El-nino, mno tuna wasiwasi, mahangaiko, ukija tutakipata

El-nino, hayo hutufika nasi, tukatoroka, nyumba zetu zikajeta

El-nino, wewe na vyako vikosi, mkitufika, mno hutupa kusota.

El-nino, mbiu yako iko nasi, washatangaza. waanza kututafuta

El-nino, tangazo tumeliasi, unavyotuliza, hutakiki katakata

El-nino, hatuamini ni sisi, utatuliza, kila mahali kutota.

El-nino, dunia huitakasi, waangamiza, nyumba zikakosa kuta.
El-nino, mafuriko ni vifusi, yatabakiza, kibomoka hizo kuta
El-nino, utawasomba farasi, mbu kujaza, na maradhi kutupata.

El-nino, twambwa mvua baraka, lakini yako, tesi kwetu sisi kitupata

El-nino, makazi huvurugika, kila ujako, na miji ikazorota

El-nino, wengi wakilipulika, latajwa lako, mawazo huwavukuta.

El-nino, kwa wengine ni mrija, fedha za uma, mbawa zipate kuota

El-nino, wakisikiya ukija, visu vya nyama, kwa usafi huvifuta

El-nino, ni lini 'taleta tija, kwa mkulima, awe bure hakupata?

**Maswali**

a) Shairi hili laweza kuainishwa katika bahari mbalimbali. Taja nne na ueleze sababu (alama 4)

b) Taja madhara yanayotokana na hali ya anga inayorejelewa. (alama 4)

c) Kwa kutoa mifano onyesha jinsi idhini ya mshairi ilivyotumika katika shairi hili. (alama 4)

d) Fafanua vipengele vinne vya muundo wa shairi hili. (alama 4)

e) Taja na utoe mfano wa tamathali mbili za lugha katika ubeti wa kwanza. (alama 2)

f) Eleza kinaya katika ubeti wa mwisho. (alama 2)

**5. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

**MSALABA MWEKUNDU**
Kofia kuvulia, msimbo nakubatiza

Tunu nakupa, saluti mi nakupigia

Nakwita awaza, ni zao la wazawa

Hukusita kufika, kunako majanga litenda jamala, kuondoza hamasa

Jitihada kudura, kufa ndo kufaana.

Shirika letu hili la msaada, msalaba mwekundu, umempiku kaka, wa majuzi kugatuliwa

Makiwa wote wa gasia, wakimbizi Somalia, umewatenda jamala, ujipatapo wajikuna

Ambulensi jaa kotekote, msalaba mwekundu, huduma kiafya, wawakimu wasojiweza

Kilioni jamaye keshafika, kaka mkubwa ajivuta, yuanazo kadhalika, atafuta lakuamba shirika katu sina wahika,

shirika lilo imara, wekundu ulokoza, ni kwa karne na mikaka

Harambeni yu fahamika, mamilioni wafikisha, juhndi zasifika, msalaba huu waimarika.

Kaka kabarikiwa, ye mwana kazaa

Kampiku kaka, habarizo pochipuka

Liwalo loandikwa, kama halipo lija

Tembo yu msalaba, ndama niye kaka

Siri yafahamika, amani kuidumisha

Msalaba watosha, ni kweli watosha.

**Maswali**

a) Thibitisha kuwa shairi hili si shairi la arudhi. (alama 4)

b) Taja faida tatu wananchi wanazopata kutokana na shirika lililotajwa. (alama 3)

c) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha nathari. (alama 3)

d) Taja fani mbili katika ubeti wa kwanza na utoe mfano. (alama 4)

e) Eleza tofauti kati ya utendaji kazi wa kaka na wa shirika la msalaba mwekundu. ` (alama 4)

f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi (alama 2)

i) Tunu

ii) Jamala

## SEHEMU YA D (Alama 20 )

### HADITHI FUPI DAMU NYEUSI

4. **Jibu swali la 6 au la 7**

**6 Kwa kurejelea hadithi zifuatazo eleza jinsi uozo ulivyokithiri katika jamii (alama 20)**

i) Damu nyeusi

ii) Mwana wa darubini

iii) Shaka yamambo.

iv) Tazamana na mauti.

**7. Gilasi ya mwisho makaburini – S.A. Mohammed. "Na wewe sharti unigande mimi tu kama kupe?"**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Taja na ufafanue mbinu mbili za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)

c) Eleza sifa tatu tatu za: (alama 6)

i) Mzungumzaji

ii) Mzungumziwa

d) Ushirikina ni mojawapo wa maudhui makuu katika hadithi hii. Fafanua kwa kutoa mifano (alama 6)

## SEHEMU YA E (Alama 20 )

### FASIHI SIMULIZI

5. 8. a) (i) Eleza miviga katika fasihi simulizi (alama 2)

(ii)Fafanua matumizi matatu ya miviga katika jamii (alama 6)

b) Matumizi ya ngomezi ya kiasili yana udhaifu wake. Fafanua. (alama 6)

c) Taja hatua mwafaka zinazoweza kuchukuliwa ili kuhakikisha fasihi simulizi itaendelea kuwepo. (alama 6)